

UTUREHEMU EE BWANA

KWARESMA

SCOUTH A.
Dodoma- Diocese
Feb, 2023.

$\text{♩} = 50$

U tu re he mu ee bwa na kwa ku wa tu tu me

te nda dha mbi bwa na tu me te nda dha mbi

13

1. Ee Mungu unirehemu sawasawa na fadhili zako, uya fute makosa yangu, unioshe kabisa na uovu wangu, unitakase dhambi zangu.
2. Maana nimejua mimi makosa yangu, na dhambi yangu I mbele yangu daima, nimekutenda dhambi wewe peke yako, na kufanya maovu mbele ya macho yako.
3. Ee Mungu uniumbie moyo safi, uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu, usinitenge na uso wako, Wala roho yako mtakatifu usiniondolee.
4. Unirudishie furaha ya wokovu wako, unitegemeze kwa roho ya wepesi, Ee bwana uifumbue midomo yangu, na kinywa changu kitazinena sifa zako.